# STANDARD FIVE YEAR 2016

# END-TERM 2,

**KISWAHILI PAPER**

**TIME: 1HR-40MINS**

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

# KISWAHILI TIME: 1HR-40MINS

**Kutoka swali la 1 hadi 15 chagua jibu sahihi**

Wawindaji haramu wanaharibu uchumi ____1____ nchi yetu. Wao ____2____ wanyama wa pori. Wanyama ____3____ wanaletea nchi yetu pesa nyingi. ____4____ huja nchini ____5____ kuwaona wanyama hawa. Siku ____6____ wawindaji hawa walikuwa ____7____ kazi yao haramu ____8____ walikuwa msituni ____9____ wawindaji hawa. ____10____ mbali waliwaona watu. Walipofika ____11____ nao waliona kuwa walikuwa majangili ____12____ wameangamiza ndovu ____13____ waliwashika na ____14____ silaha zao ____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. wa | C. la | D. za |
| 2. | A. wanauwa | B. wanawauwa | C. wanaua | D. wanawaua |
| 3. | A. hizi | B. huyu | C. hawa | D. haya |
| 4. | A. Wakimbizi | B. Watalii | C. Watoro | D. Walowezi |
| 5. | A. mwetu | B. yetu | C. letu | D. wetu |
| 6. | A. moja | B. mumoja | C. mmoja | D. monja |
| 7. | A. kwa | B. na | C. katika | D. kwenye |
| 8. | A. maskani | B. mapolisi | C. polici | D. askari |
| 9. | A. wakiwaficha | B. wakiwatafuta | C. wakiwalinda | D. wakiwasumbua |
| 10. | A. kwa | B. na | C. pa | D. mwa |
| 11. | A. mbali | B. kando | C. nyuma | D. karibu |
| 12. | A. walikua | B. hawakua | C. walikuwa | D. hawakuwa |
| 13. | A. mawili | B. mbili | C. miwili | D. wawili |
| 14. | A. kuwanyanganya | B. kuwanyang'anya | C. kuwapa | D. kutupa |
| 15. | A. sote | B. zote | C. yote | D. lote |

**Swali la 16 hadi 30 jibu kulingana na maagizo**

16. Mzazi wa kiume utamwitaje?
A. Babu B. Baba C. Kaka D. Mzazi

17. Juma ni ____ kuliko Yohana.
A. safi B. nzuri C. mhondari D. msafi

18. Ni sahihi kusema____
A. Mtoto hakuli B. mtoto hali
C. mtoto hakukula D. mtoto hakulangi

**Kamilisha**

19. Mwanafunzi ______ analia ni mpumbavu.
A. mwenye B. mwenyewe
C. ambaye D. ndiye

20. Kifaa kinachotumiwa na seremala kupima urefu au ufupi ni ______
A. pembe mraba B. kekee
C. utepe D. bisibisi

21. Mwezi wa tano wa mwaka huitwa ____?
A. Mai B. Meyi C. Aprili D. Mei

22. **Andika umoja:**
Maswali haya ni magumu.
A. swali hii ni gumu. B. swala hili ni ngumu.
C. swali hili ni ngumu. D. swali huyu ni ngumu.

23. Anayetunza vitabu maktabani huitwa?
A. mhasibu B. mkurugenzi
C. mkutubi D. malenga

24. Mzoga wa mbwa unanuka______!
A. fyu B. fye C. fe D. po

**Kamilisha methali**

25. ______ hayana pazia.
A. Macho B. Madirisha
C. Milango D. Masikio

26. Ni nini kinyume cha jogoo?
A. koo B. kuku C. jimbi D. pora

27. Mdudu ambaye ana miguu mingi sana duniani ni__________?
A. konokono B. kiwavi
C. jongoo D. buibui

28. Mpunga ni mimea unaotupa ______
A. ndizi B. kahawa C. mchele D. sukari

29. Magari yana ______
A. miguu B. kwato C. magurudumu D. nyayo

30. Amevalia rinda jeupe kama_____
A. barafu B. mpingo
C. nyundo D. theluji



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

**Soma Barua ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40**

**Shule ya Msingi ya Bidii**
**Sanduku la Posta 443,**
**KERICHO.**
**15/10/2012**

**Kwa rafiki Mwala,**

Natoa salamu nyingi sana kutoka kwetu hapa mjini. Wewe hujambo ulipo? Je, masomo yaendeleaje?

Hapa tunafanya bidii sana katika masomo yetu, kaka anajitayarisha kwa mtihani wake wa darasa la nane. Mimi na dada yangu tunasoma sana ili tus shindwe na wenzetu darasani. Mwisho wa muhula uliopita nilishikilia nafasi ya tatu. Baba, mama na wajomba wote walifurahi sana. Walinipa zawadi, wajomba wote walifurahi sana, walinipa zawadi.

Wasalimie wazazi, ndugu na marafiki zako. Tafadhali niandikie barua upatapo waraka huu.

Ni rafiki yako,
**Opeo Maruti.**

31. Barua hii iliandikwa na nani?
A. Mwala B. Mzazi C. Opeo D. Dada
32. Unafikiri kuwa barua hii iliandikwa muhula gani?
A. wa pili B. wa tatu
C. wa kwanza D. Octoba
33. Kulingana na taarifa mwandishi ______
A. anafanya bidii B. ni mzembe
C. anavurita mkia D. ni mjinga
34. Mwandishi alikuwa nambari tatu lini? Mwisho wa muhula wa ______
A. kwanza B. pili C. tatu D. mwaka
35. Jina jingine la barua kulingana na taarifa hii ni?
A. anuani B. muhula C. bidii D. waraka
36. Jina la mji ulioko karibu sana na mwandishi ni
A. Kericho B. Mwala C. Ulao D. Opeo
37. Nani anayejitayarisha kufanya mtihani wa darasa la nane?
A. Mwala B. Kakaye Opeo
C. Dada ya Mwala D. Maruti
38. Mwala alipewa zawadi na nani?
A. baba, mama, shangazi
B. mama, shangazi, wajomba
C. shangazi, mama, mjomba
D. wajomba, mama, baba
39. Jibu la hujambo ni ______
A. maharaba. B. sijambo
C. hatujambo D. mzuri
40. Taarifa hii ni mfano wa ______
A. hotuba
B. barua rasmi
C. barua ya kinyumbani
D. barua ya kirafiki

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 41-50**

Siku moja Josho alipokuwa akitoka shuleni alishikwa na kikohozi. Usiku huo alikohoa sana. Keshoye mama yake alipeleka hospitalini.

Daktari alimkagua na kumpa dawa iliyokuwa katika chupa. Daktari alimwambia Josho awe akitikisa chupa kabla ya kuinywa dawa.

Baada ya siku mbili Josho alikunywa dawa hiyo bila kutikisa chupa. Mara tu alipokumbuka masharti ya daktari alimwita dada yake. Alimwambia dada yake amtikise kama chupa ya dawa.

Mama yake aliingia na akauliza kwa nini Josho alikuwa akitikiswa. Josho alimjibu kuwa ni kwa sababu aliinywa dawa bila kutikisa chupa ndipo akaamua akitiswe ili dawa ichanganyike tumboni.

Mama yake alimwambia kuwa ni hatari kusahau masharti ya daktari kwa sababu kunaweza kusababisha madhara makubwa zaidi.

41. Josho aliugua nini?
A. kuhara B. kuendesha
C. kusahau D. kukohoa
42. Josho alititiwa na daktari?
A. alipewa vidonge
B. alidungwa sindano
C. alipewa dawa ya majimaji
D. alipasuliwa
43. Josho alisahau kufanya nini?
A. kunywa dawa
B. kutikisa baada ya kunywa dawa
C. kutikisa chupa baada ya kunywa dawa
D. kutikisa chupa kabla ya kunywa dawa
44. Dada yake Josho aliamuriwa kufanya nini?
A. kutikisa chupa B. kumtikisa Josho
C. Kuitikisa dawa D. kumtikisa mama
45. Josho alikuwa kitoka wapi alipougua?
A. Shuleni B. Sokoni C. Hospitalini D. Kucheza
46. Kusahau masharti ya daktari kunaweza kusababisha ______
A. faida B. furaha C. madhara D. mapenzi
47. Jina jingine la daktari ni ______
A. nahodha B. tabibu C. rubani D. mhadhiri
48. Mama alipoingia chumbani alikuta ______
A. Josho akinywa dawa
B. Josho akimtikisa dada yake
C. Josho akitikswa
D. Josho alitetemeka
49. Josho alikuwa ______
A. mpole B. mcheshi C. mwerevu D. mjinga
50. Taarifa hii inatufundisha ______
A. tuzingatie masharti tunayopewa
B. tusifuate maagizo
C. Towe wasaulifu
D. Tupuuze masharti tunayopewa



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27